# Kanisa Lililodanganywa Na Ulimwengu

Yesu Kristo, Mwana Wake, na ametupa vitu vyote bure katika Kristo. Tu wenye shukrani Kwako, Bwana, kwa majaliwa tuliyopewa na hii Dhabihu kuu kabisa aliyoitoa Yesu kwa ajili yetu pale Kalvari, iliyotupatanisha tena katika ushirika na kupendelewa Nawe, ili tuweze kuwa na faraja hii ya kujua kwamba imeandikwa, "Ninyi mkikaa ndani Yangu, na Maneno Yangu ndani yenu, mwaweza kuomba mtakalo nanyi mtatendewa." Sasa, twashukuru kwa jambo hili, na twaomba kwamba Wewe utatupa imani ya kuamini hili kwa kila kilichomo ndani yetu.

2 Sasa hebu tuweke kando, Bwana, kila shughuli ya siku hii, kila masumbufu ya maisha haya, kuanzia kwa bawabu hadi mchungaji, ili kwamba tusiwe na lolote katika nia zetu sasa, isipokuwa kungojea, kusikiliza kwa unyenyekevu Roho Mtakatifu anene nasi, ili tuweze kutimiza jambo jema, kukujua Wewe zaidi, kwa kukusanyika kwetu pamoja. Maana, Bwana, hakika hiyo ndiyo sababu tumekuja siku hii ya joto. Nena nasi kwa Neno Lako lililo hai, na Neno hai likae ndani yetu na kudumu ndani yetu, ili tuweze kuumbika na kutengenezeka, si kwa jinsi ya ulimwengu, lakini tugeuzwe kwa kufanywa upya roho zetu, katika mfano wa Mwana wa Mungu. Loo, mioyo yetu inatetemeka tunapowaza, na furaha inafurika katika nafsi zetu, kujua kuwa tunaweza kuitwa wana na binti za Mungu. Na tunasimama ukingoni kabisa wa Kuja Kwake Mara ya Pili, na mataifa yote na falme zote zinatetema chini ya miguu yetu, vitu vyote vya dunia hii vinatoweka, lakini tunajua kuwa siku fulani Yeye atakuja na atatupeleka katika Ufalme ambako kamwe hakutakuwa na mwisho, au, kamwe hautaondolewa. Na tukiwaza kuwa sasa sisi ni—ni raia wa huo Ufalme! Ee Mungu, tahiri mioyo yetu na masikio yetu leo, kwa—kwa Roho Mtakatifu, kwa kuoshwa kwa maji ya Neno. Maana tunaomba hivi katika Jina Lake na Kwa utukufu Wake. Amina.

3 Nataka kuliendea somo asubuhi hii. Kwa kuwa, ilikuwa nizungumze juu ya jambo tofauti kidogo, kama pangekuwa na ibada ya uponyaji, lakini tulitangaza kwamba kadi za maombi zitolewe saa mbili, hadi saa mbili na nusu au saa tatu. Nami tu. . .Billy alikuja nyumbani dakika chache zilizopita na akasema hapakuwa na mtu ye yote hapa, hivyo hakugawa kadi za maombi. Kwa hiyo tuta. . .Niliwaza kuchukua somo hili, kwa masahihisho ya kanisa. Nami nataka kuzungumza kuhusu somo la: *Kanisa Lililodanganywa Na Ulimwengu*. Nataka kusoma

sehemu sasa katika Kitabu cha Waamuzi sura ya 16, kuanzia aya ya 10.

> *Delila akamwambia Samsoni, Tazama, umenidhihaki, na kuniambia uongo; sasa niambie, tafadhali,* waweza kufungwa wapi.
>
> *Naye alimwambia,* Ukinifunga *tu kwa kamba mpya ambazo hazijatumika bado, hapo ndipo nitakuwa dhaifu, nitakuwa kama mtu mwingine.*
>
> *Basi Delila alitwaa kamba mpya akamfunga nazo, akamwambia, Wafilisti wanakujia, Samsoni. Na walikuwako wale wenye kuotea katika chumba cha ndani. Naye akazikata na kuzitupa kutoka mikononi mwake kama vile* ni nyuzi.
>
> *Delila akamwambia Samsoni, Hata sasa umenidhihaki, umeniambia maneno ya uongo; niambie waweza kufungwa* wapi wewe. *Akamwambia, Ukivifuma...vishungi saba vya nywele za kichwa changu katika mtande wa nguo.*
>
> *Basi akazifunga kwenye* misumari, *akamwambia Samsoni, Wafilisti wanakujia. Naye akaamka usingizini, akang'oa* ile misumari ya zile nguzo*, na ule mtande.*
>
> *Mwanamke akamwambia, Wawezaje kusema, Nakupenda, na moyo wako haupo pamoja nami? umenidhihaki mara hizi tatu, na ume...niambia asili ya nguvu zako nyingi, wala hukuniambia asili ya nguvu zako nyingi.*
>
> *Ikawa, kwa vile alivyomsumbua kwa maneno yake kila siku, na kumuudhi, roho yake ikadhikika hata kufa.*
>
> Na *ndipo alipomwambia yote yaliyokuwa moyoni mwake, akamwambia, Wembe haujapita kichwani mwangu kamwe; maana nimekuwa Mnadhiri wa Mungu, tangu tumboni mwa mama yangu; nikinyolewa, ndipo nguvu zangu zitanitoka, nami nitakuwa dhaifu, nitakuwa kama wanadamu wengine.*
>
> *Delila alipoona ya kuwa amemwambia yote yaliyokuwa moyoni mwake, akatuma mtu akawaita... wakuu wa Wafilisti, akisema, Njooni huku mara hii tu, maana* amenionyesha *yote aliyo nayo moyoni mwake.* Na *ndipo wakuu wa Wafilisti wakamwendea, na wakatafuta ile fedha* au *wakachukua ile fedha mkononi* mwake.
>
> *Naye akamlaza usingizi* gotini *pake; kisha akamwita mtu, naye akavinyoa vishungi saba vya nywele za kichwa chake; a...akaanza kumsumbua, nguvu zake zikamtoka.*

*Kisha akasema, Samsoni, Wafilisti wanakujia. Akaamka katika usingizi wake, akasema, Nitakwenda nje kama siku nyingine, na kujinyosha. Lakini hakujua ya kuwa BWANA amemwacha.*

4 Sasa nataka kusoma, kwa kupata kiini cha somo hili, kutoka Kitabu cha Ufunuo, sura ya 2, kuanzia aya ya 21 na ya 23.

*Nami nimempa muda ili autubu, wala hataki kuutubia* uzini wake.

*Tazama, nitamtupa juu ya kitanda, na hao wazinio pamoja naye, wapate dhiki kubwa wasipotubia matendo* yao.

*Nami nitawaua watoto wake kwa mauti. Na makanisa yote watajua ya kuwa mimi ndiye achunguzaye viuno na mioyo. Nami nitampa kila mmoja wenu kwa kadiri ya matendo yake.*

Bwana aongeze baraka Zake katika kusoma Neno Lake.

5 Samsoni, anayefanana sana na kanisa, alianza vizuri. Alianza kwa mwelekeo sahihi. Alianza, naye aliitwa mtu mkuu aliye shujaa. Lakini alianza kwa kumtumikia Bwana, kwa kushika Maneno Yake na kutimiza Amri Zake. Na hapo kidogo alikuwa kama kanisa. Lilipoanza, tungesema, kwa msemo wa kilimwengu, lilianza vyema. Lilianza kwa kushika Amri za Bwana. Na maadam Samsoni alimfuata Bwana, Bwana alimtumia Samsoni.

6 Maana, Mungu aweza kumdumisha yeyote na kumtumia yeyote atakayemfuata Yeye, kwa kuwa hiyo ni kazi Yake Mungu. Lakini tukigeuka kando, mbali na mambo ya Mungu, hapo Mungu hawezi kututumia tena. Wakati tutakapofuata kwa uthabiti Amri za Mungu, wakati tutakapokaa katika kurasa za Biblia na kuabudu kwa Neno lililoandikwa, tukimwabudu Yeye katika Roho na katika Kweli ya Neno; ndipo Mungu aweza kumtumia mtu yeyote. Lakini pindi wakichukua wazo la kugeuka kando kwa kufuata kitu kingine, ndipo Mungu hawezi kumtumia mtu huyo tena.

7 Hivyo, Samsoni anakuwa mfano m—mzuri sana wa kanisa la leo. Wakati kanisa lilipoanza, Mungu aliweza kulitumia kanisa, maana kanisa lilizingatia kwa uangalifu Amri za Bwana, lilishika hukumu Zake zote na maagizo Yake, na kuzitenda Amri Zake zote. Na Mungu alikuwa pamoja na kanisa. Lakini inaonekana kuwa kuna mahali pa kudhoofisha sana kati ya kanisa.

8 Kumbuka, hatuko kwenye mandari, lakini tuko katika uwanja wa vita. Watu wengi hudhani kuwa wakati wanapokuwa Wakristo kwamba ni hilo tu wanalohitaji kufanya, kwamba hilo latosha milele, maadamu ni Wakristo kila kitu kitakuja kwa urahisi. Kamwe usiweke hilo kichwani mwako. Maana,

ninakuwa Mkristo, kupigana, nipigane vita vizuri vya imani. Ninakuwa Mkristo, niingie katika mstari wa vita. Sisi ni askari Wakristo, na yatubidi kufundishwa na kuzoezwa na kujua mbinu zote za yule adui, kujua namna ya kujikinga, kujua namna ya—ya kupigana vita. Na tunaweza kufanya hivyo tu jinsi Roho Mtakatifu atakavyotufunulia hayo. Hatuwezi kuchukua yale taifa jingine linatuambia tuendapo vitani, baadhi ya mawazo yao. Lakini yatubidi kuchukua mawazo yetu, jinsi Roho Mtakatifu angetuongoza, na mawazo yale Yeye angetupa, kwa sababu Yeye ni Amri Jeshi wa jeshi la Wakristo.

9 Samsoni alifanya vema, alikuwa mtu mkuu hadi alipoanza, alianza (tungaliita) kufanya uzembe, hadi alipoanza kuvuka jimbo lake mwenyewe. Na kanisa lilipiga mbio vema, na lilikuwa sawasawa hadi walipoanza kuvuka jimbo lao. Samsoni alianza ubembe. Na hakuwa anabembana na wasichana wa Israeli, alianza kubembaana na wasichana Wafilisti.

10 Na hilo kidogo ni sawa na kile kanisa lilifanya. Halikufanya mapenzi na walio wake, liliwafuata wasioamini na kuanza kubembana na wasioamini. Hapo ndipo tulijifanyia makuu, na mojawapo ya makosa makuu kabisa, ni wakati kanisa lilianza kufanya mambo yasiyo sahihi. Lilianza kuwa, kama Samsoni, na marafiki wabaya.

11 Samsoni, maadamu alikuwa katika ushirika wa watu wa Bwana alifanikiwa. Lakini alipoanza kubembana na marafiki wabaya, ndipo alipata matatizo.

12 Na hivyo ndivyo ilivyo kwa kanisa. Wakati kanisa lilifuata kwa unyenyekevu na kila siku uongozi wa Roho Mtakatifu, Mungu aliwabariki, na miujiza na ishara na maajabu vilifuata kanisa. Lakini lilipoanza kuambatana na kundi baya, na ulimwengu! Mojawapo ya mambo mabaya kabisa liliyofanya, na mambo ya kwanza liliyofanya, lilianza kuunda madhehebu, kuvunja ushirika miongoni mwa waaminio wengine, kwa sababu walipata kujua kwamba mataifa waliunda madhehebu. Lakini hii Injili kuu haikuwekwa wakfu kwa ajili ya taifa moja au watu wa tabaka moja. Imewekwa wakfu kwa "yeyote atakaye, na aje," mataifa yote, jamaa, lugha, na watu. Kamwe Mungu hakukusudia sisi tuweke mipaka.

13 Lakini watu walitaka kuwa kama, walijilinganisha, au kuigiza, kuenenda kama u—ulimwengu unavyofanya, kusema mambo wasemayo, kufanikiwa jinsi walivyofanikiwa. Hatuwezi kamwe kufanikiwa kwa kufanya lolote linalofanywa na ulimwengu. Tunaweza kufanikiwa tu kwa kufuata sheria za Mungu na njia Yake ya kufanya mambo. Kamwe hatuwezi kuwa, kwa kujifananisha na ulimwengu. Ikiwa kampuni ya sigara wamepata mafanikio yao makubwa kabisa kwa televisheni, na ya bia na makampuni ya wiski wamepata mafanikio yao makubwa kwa njia ya televisheni, hiyo siyo ishara kwamba

kanisa litapata mafanikio kwa televisheni. Mafanikio ya kanisa yanakaa katika kuhubiri Injili, ya Uweza wa Mungu, na dhihirisho la Roho. Hatuwezi kusema eti kwa sababu televisheni imefanya hivi na hivi kwa kampuni ya sigara na—na makampuni mengine! Hatuna Andiko lolote kujaribu kujilinganisha na hao watu. Na maadamu tunafanya hivyo, tunaweza kuvuta hesabu kubwa ya watu, lakini hivyo sivyo Mungu alituamuru kufanya. Tunadhani kuwa kwa sababu wote tumefanikiwa sana, tumestawi, madhehebu makubwa, tunaweza kufanya mambo makuu ya kuvutia yotokee, ati kwamba ni mafanikio. Tunakufa hali tumesimama kila siku, nikizungumza kiroho! Kama tungesimama pamoja watu milioni kumi asubuhi hii, na Roho Mtakatifu hakuwa pamoja nasi, tungefanya vema kusimama pamoja watu kumi na Roho Mtakatifu akiwa pamoja nasi. Hatuwezi kujilinganisha na ulimwengu.

14 Na mojawapo ya mambo ya kwanza, ilikuwa, kanisa kujiundia madhehebu. Madhehebu ya kwanza ni kanisa la Katoliki, na ndipo likaja kanisa la Kiluteri. Wakati walipounda kanisa la Katoliki kulifanya madhehebu, siku moja kulikuwa na kilio, "Wafilisti wanakujia, Samsoni," naye Samsoni akakata kamba za vifungo vya kanisa la Katoliki, na Martin Luther akatokea na madhehebu.

15 Ndipo walilifunga kanisa kwa kamba nyingine, kama alivyofanya Delila. Na walianza. . .badala ya kuwa na watu walioitwa na Mungu, watu walioitwa na Roho Mtakatifu, huenda hawakujua herufi zao za ABC, lakini walimjua Kristo. Ndipo kanisa lilichukua mitindo, na kujifananisha na wanenaji wa kisiasa. Na iliwabidi kuwapa wahubiri wao "shahada za daktari," kila mmoja ilibidi awe Daktari wa Elimu ya Kiungu. Hiyo ilikuwa ni kamba nyingine ya kulifunga kanisa. Watu wakaenda kusoma, kila seminari inajaribu kutoa mwanachuoni bora, ili makanisa yao yaweze kujisifu, "Mchungaji wetu ni Daktari wa Elimu ya Kiungu." Na, walifanyaje, mmoja hujaribu kupata maarifa zaidi ya mwingine. Naam, haya hayana maana yoyote machoni pa Mungu.

16 Na hakuna haja kwa mtu yeyote kujaribu kuchukua maarifa yake ya kilimwengu ili kumpendeza Mungu kwa hayo. Ni machukizo machoni pa Mungu! Hutampendeza Mungu kamwe kwa tamaa za ulimwengu na maarifa yake, kwa sababu "ni uadui kwa Mungu," yanena Maandiko. Hawezi kufanya hivyo.

17 Na kila mtu anajaribu kupata maarifa yote. Wanajua tu la kufanya na maneno ya kusema, na inakuwa tu hotuba ya kisiasa badala ya Ujumbe wa Roho Mtakatifu unaodhihirishwa katika nguvu, unaozama katika moyo wa mwanadamu na kuifichua dhambi. Wamefundishwa kwa usemaji wa kisiasa, na hatuhitaji huo. Paulo alinena, "Neno limekuja kwetu, siyo tu kwa. . .au, Injili, katika Neno tu, bali kwa Nguvu na dhihirisho la Roho Mtakatifu." Hiyo ilileta Injili, ikidhihirisha uweza wa Roho

Mtakatifu! Lakini watu wote hawa wanakwenda seminari na kujifunza elimu kubwa, jinsi ya kusimama mbele za watu, jinsi wanavyopaswa kwenda mbele za watu, jinsi wanavyopaswa kuvalia na jinsi wanavyopaswa kutenda, kamwe hawapaswi kukosea sarufi. Sasa, hiyo ni sawa kwa hotuba ya kisiasa, lakini hatutafuti maneno ya kushawishi ya kibinadamu. Paulo alinena, "Injili ninayohubiri haikuja kwa jinsi hiyo, lakini ilikuja kwa kufanywa upya na—na Roho Mtakatifu, na Nguvu za dhihirisho." Haiji kwa hotuba iliyotungwa kwa usahihi, ili hekima yenu ingalikuwa, au tumaini lenu liwe katika hekima ya kibinadamu. Lakini inakuja kwa madhihirisho ya Nguvu za Kristo aliyefufuka. Hiyo ndiyo Injili, "Kumjua Yeye katika Nguvu za kufufuka Kwake."

18 Kila mmoja anajaribu kufikiri ni stadi zaidi kidogo kuliko mwenzake, kila dhehebu. Wamethodisti watasema, "Tunaye mtu stadi kuliko wote." Wabatisti watasema, na Church of Christ, na wengineo, hao wote, "Sisi, sisi ni stadi kuliko wote. Sisi wa—watu wetu, hatuachi mtu wa kawaida aende akahubiri Injili." Lakini wanawachagua. (Ee Mungu, rehemu!) Wanawachagua, ikiwa wameelimishwa katika fundisho lao maalum, ndipo huwaweka kanisani. Mungu hawezi akagusa hilo kwa njia yo yote, nataka kuhubiriwa na mtu aliyechaguliwa na Roho Mtakatifu. Aliyeinuliwa na Mungu, siyo aliyechaguliwa na binadamu au madhehebu.

19 Maarifa yote! Wao husema, "Loo, tunajua Yote," na baadhi yao hawajui herufi ya kwanza ya Roho Mtakatifu. Wanaikana.

20 Inanikumbusha kitabu kidogo nilichosoma siku moja huko California, yapata miaka kumi iliyopita. Nilikichukua katika duka la vitabu vilivyotumiwa. Nimesahau nani alikuwa mwandishi. Kitabu kidogo tu cha senti kumi, lakini kilikuwa na busara ndani yake ingawa kilionekana ni cha utani na hila. Lakini, nilipata kitu ndani yake kilichosikika kama Mungu kwangu. Na moja ya hadithi hizo fupi ilianza hivi. Asubuhi moja katika banda kubwa la kuku kulikuwa na jogoo fulani mdogo, ambaye alidhani ana maarifa yote yaliyohitajika kujulikana. Hivyo aliruka juu ya sanduku na akapiga mdomo wake mdogo kwenye hilo sanduku, mara nne au tano, akarusha nyuma kichwa chake kidogo na kuwika kwa namna ambayo hujawahi kusikia jogoo akiwika. Na wengine, akavuta usikivu wao, naye akasema, "Mabibi na mabwana wa banda hili la kuku, ningependa kuzungumza nanyi nyote asubuhi hii kuhusu mpango mkubwa wa elimu tulioutayarisha hivi karibuni." Akasema, "Nimepata maarifa kwa wingi katika kujifunza kwangu," alipokuwa akivuta miwani yake midogo juu ya mdomo wake. Naye akasema, "Nimeamua kwamba sisi kuku tunaweza kujinufaisha kwa maarifa zaidi. Kwa hiyo, naweza kuwaambia ambapo kwamba, ikiwa tutachimba na kushughulika katika banda au tundu fulani, tutapata vitamini fulani ambayo

itatufanya tuwike vema, manyoya mazuri zaidi. Na, lo, naweza kuwaambia jinsi tutakavyoweza kujinufaisha kwa njia nyingi mbalimbali."

21 Na wale kuku wadogo wenye nyundu dogo nyekundu, wakatetea na kusema, "Je si mzuri sana huyu?" Na kwa hakika wakampenda. "Loo, ni jogoo mwenye akili sana!" Yanikumbusha baadhi ya hawa wahubiri wa seminari. "Mtu wa akili namna hii! Hapana haja ya sisi kubakia hapa na kuku wengine, wote yatubidi kwenda naye."

22 Naam, kabla yule jamaa mdogo hajamaliza hotuba yake, kulikuwepo na kuku mwingine mdogo asiyekuwa na manyoya mang'avu hivyo, akaja anakimbia kutoka katika sehemu nyingine ya uwanja wa kuku, na akasema, "Jamani, ngojeni kidogo! Nimesikia habari za karibuni sana katika redio. Kuku wamepanda bei kwa senti nne kwa ratili, sote tutakwenda kichinjioni kesho! Maarifa yako yatakuwa na faida gani?"

23 Ndugu, maarifa yote ambayo tunaweza kukusanya, yanafaa nini? Sisi ni futi sita za uchafu! Sote tunakufa kwa inchi na kwa dakika. Maarifa yetu hayana maana yo yote. Tunataka kumjua Yeye. Lakini wao wanafanya hivyo.

24 Kama nilivyokuwa nasema muda kitambo uliopita kuhusu kurumbizi fulani mdogo, na alidhani kuwa alijua maarifa yote ambayo—ambayo yanafaa kujulikana, na alijua mengi hivi kwamba angeweza kuwaambia kurumbizi wengine wote kuhusu wanadamu. Hivyo akaruka juu kwenye kizimba chake na akaanza kuzungumza kuhusu wanadamu, jinsi alivyofahamu yote yanayowahusu. Na kwa ghafla, profesa kutoka Purdue akatokea na kuanza kumzungumzia maneno yenye ufasaha, na huyo jamaa mdogo akaanza kupepesa macho yake na kugeuza kichwa chake. Sasa, alikuwa na macho, angeweza kumwona profesa. Alikuwa na masikio, angeweza kumsikia. Lakini, bila shaka, hakujua yale alikuwa anazungumzia. Kwa nini? Ana ubongo wa kurumbizi. Yeye ana ubongo wa ndege tu. Hicho tu ndicho alicho nacho. Hana ubongo wa mwanadamu, hivyo hawezi akawaza kama wanadamu.

25 Wala binadamu hawezi akawaza kama Mungu! Wewe ni mwanadamu, na maarifa yote ya ulimwengu siyo zaidi ya ubongo wa kurumbizi. Yote unayoyafanya, unajiumiza nayo mwenyewe. Unapaswa kuwa na nia ya Kristo.

26 Sababu ya watu kwenda na kujiunga na madhehebu, na kupeana mikono badala ya kuzaliwa upya, wanajaribu kuepuka kuzaliwa upya. Hawataki kuzaliwa upya. Na wana—wanajua tunalifundisha katika Biblia, hivyo wanataka kuweka kitu fulani badala yake. Na watu wa Pentekoste ni wabaya vivyo hivyo, wakijaribu kuweka kitu fulani badala yake! Wanataka iwe katika daraja. Sharti iwe ya daraja ya juu, "Tutapeana mikono na kujiunga na kanisa, na kunyunyuziwa

au kubatizwa," au kitu kingine. Wanaogopa kuzaliwa upya. Wakati mwingine naamini kuwa Maskani ya Branham wanaanza kuogopa jambo hilo!

27 Sasa, sote tunajua kwamba kuzaliwa, sijali ni wapi, au wapi, mahali gani, ni mchafuko. Kama mtoto akizaliwa kwenye lundo la makapi, kwenye sakafu ngumu, au katika chumba cha hospitali kilichonakshiwa kwa rangi ya zambarau, ni mchafuko, hata hivyo. Kuzaliwa kwa ndama, kuzaliwa kwa kingine cho chote, ni mchafuko.

28 Na kuzaliwa upya ni mchafuko vivyo hivyo! Lakini watu ni wagumu sana, "Tutakwenda mahali wanapopeana mikono. Tutakwenda mahali wasipopiga kelele na kulia, na kupigapiga mimbara na kupaza sauti." Mnataka kuwa na ubinadamu mno! Tunachohitaji ni kuzaliwa, kufa, ili kuleta Uzima!

29 Mbegu, kiazi kikuukuu, mbegu ya kiazi, chukua kile kiazi na ukipande katika udongo. Mpaka uweze kupata viazi vipya, hicho kiazi kikuukuu itapasa kioze. Hindi haliwezi kutoa uhai mpya mpaka limeoza.

30 Na mwanamume au mwanamke hawezi kuzaliwa upya mpaka ufahamu wao na ubinafsi wao umeoza, ukafa, ukafa madhabahuni, na kupiga yowe, uchafuliwe kwa kila hali, hata kufikia mahali ambapo ugumu umetoka kwenye ukosi, nawe umezaliwa upya kwa Roho wa Mungu. Sijali iwapo utapiga kelele, utanena kwa lugha, utarukaruka juu chini, upapatike kama kuku aliyekatwa kichwa, unaleta Uhai mpya! Lakini tuliweka kitu kingine badala yake, tunataka njia ya daraja bora, hakika.

31 Hivi majuzi, Ijumaa, mimi na mke wangu tulikuwa tunakwenda dukani. Sikusudii kurudiarudia hili. Lakini tulipokuwa tunatembea barabarani, niliendelea tu kugeuza kichwa changu huku na huko, wanawake walikuwa uchi. Nilimuahidi Mungu nilipokuwa kipofu, kwamba ikiwa angeponya macho yangu ningeangalia lile lililo la haki. Nami nimeweka msalaba mdogo unaoning'inia ndani ya gari langu. Nionapo mambo ya aina hiyo, huangalia msalaba na kusema, "Ee Mungu, Huo ndio Kimbilio langu," niangaliapo ule msalaba.

32 Niliwaona wale wanawake. Meda alisema, "Hatujaona mwanamke hata mmoja leo aliyevaa rinda." Na alisema, "Bill, angalia mwanamke yule pale na ile mikanda midogo aliyoifunga juu ya mwili wake," akasema, "unataka kuniambia yule mwanamke hajui kuwa hilo ni kosa?" Akasema, "Kama hajui kuwa ni kosa, basi hana akili timamu."

33 Nilisema, "Ngoja kidogo, mpenzi. Yeye ni Mwamerika, anatenda kama Waamerika watendavyo." Nilisema, "Nilikuwa Finland siyo muda mrefu uliopita, mpenzi."

34 Na pale nilimuuliza mtu aliyeniketisha chini, Daktari Manninen. Tulikuwa tunakwenda kwenye—kwenye hamamu,

inayoitwa sauna, na wao hukuingiza ndani na kumwagilia maji moto, au maji juu ya miamba ya moto, nayo hukufanya wewe utoke jasho. Ndipo hukufanya ujichovye ndani ya maji ya barafu, na tena utoke. Ndipo hukupeleka ndani ya chumba, na humo kuna wauguzi, wanawake wanaowasugua hao wanaume (nao wakiwa uchi), na kuwarudisha katika kile kidimbwi. Singeingia humo. Na nilisema, "Daktari Manninen, hilo ni kosa."

35 Alisema, "Sawa basi, Kasisi Branham, hilo ni kosa. Basi vipi kuhusu madaktari wenu Waamerika watakaomvua mwanamke nguo abaki uchi kisha wamlaze juu ya meza, wakague kila kiungo cha uke alicho nacho? Vipi kuhusu wauguzi wenu katika mahospitali?"

36 Nilisema, "Niwie radhi, Ndugu Manninen, Manninen, umesema kweli."

37 Ni nini? Ni desturi. Nilipokuwa Paris ilikuwa vigumu kuamini hili, kwamba mahali pa kukojoa kwa wanaume na wanawake palikuwa ni pamoja. Sikuweza kuelewa hili, kwamba msala ulikuwa kandokando ya barabara kwa ajili ya wanaume na wanawake pamoja. Sikuweza kuamini kwamba wakati wanawake walikwenda ufukoni kuogelea, mvulana na mpenzi wake, hawana vyumba vya kubadilishia mavazi, walivua nguo zao zote hadi vazi la mwisho, ndipo hugeuza migongo yao na kuvaa ukanda mdogo na kwenda kuogelea, lakini ndivyo ilivyo. Hawajali hilo. Ni desturi ya Ufaransa.

38 Katika Afrika, wanawake na wanaume, vijana kwa wazee, hawana nguo kabisa, wanatembea mbugani. Hawajui kabisa msalani ni nini, au mengineyo, au hamna aliyekwenda mbali na mwenzake. Lakini hawajui vinginevyo. Hawajui vinginevyo. Bali ni desturi za mataifa.

39 Lakini nilisema, "Mpenzi, sisi ni tofauti, tunatoka Taifa jingine. Sisi ni wasafiri na wageni hapa, hiyo ndiyo inayafanya mambo haya yaonekane makosa hivi. Maana Biblia ilisema, 'Wao ambao wanashuhudia haya, wanaoadai, wanaonyesha kwamba wao ni wasafiri na wageni, wanautafuta mji ujao.'"

40 Mwanaume au mwanamke katika Italia, katika Ufaransa, katika Afrika, katika taifa jingine lolote, aliyezaliwa upya na Roho Mtakatifu, hafanyi mambo hayo. Hawatavaa hizo nguo. Hawatatenda mambo ya jinsi hiyo, kwa sababu ni wa Taifa jingine ambalo Mtawala na Mjenzi Wake ni Mungu. Tumetoka Mbinguni. Roho iliyomo ndani yako, inaendeleza maisha yako. Kama wewe ni Mwamerika, utatenda jinsi Waamerika watendavyo. Kama wewe ni Mfaransa, utatenda jinsi Wafaransa watendavyo, na kumlaumu yule mwingine. Lakini kama wewe ni wa Mungu, utatenda jinsi watendavyo Mbinguni, kwa sababu Roho wako anatoka Juu na anakutawala wewe.

41 Kitu fulani kidogo unachoweza kukiangalia. Katika Maandiko, wale walioutafuta huu Mji mpya, walitenda tofauti.

Walikiri kwamba walikuwa wasafiri na wageni. Lakini ule upande wa Kaini, wanakuwa watoro na wahaini. Lakini Wakristo walikuwa wasafiri na wageni. Mtoro hana makao, haini ni mtu fidhuli. Lakini msafiri ni kitu halisi, na kutoka nchi halisi katika Taifa jingine, akijaribu kutafuta njia ya kwenda Nyumbani, akishuhudia kwa maisha yake kwamba anacho kitu kionyeshacho kuwa anatoka Nchi nyingine. Hiyo ndiyo sababu yake.

42 Hata hivyo hao watu wafanyao hayo, hao watu wavaao vitu hivyo, hebuni nikwambie. Katika Afrika ya Kusini, nilipoona makafiri kwelikweli elfu thelathini, walio uchi, wenyeji wavaao mablanketi. Wasichana na wavulana wa umri wa miaka kumi na sita, kumi na nane, hadi ishirini wasio na hata kipande cha nguo, wakisimama hapo na matope nyusoni mwao, na wamejipodoa, mifupa katika pua zao, na vipande vya miti vikining'inia katika masikio yao, mifupa ya wanadamu iliyopitana au baadhi ya mifupa katika nywele zao, meno ya wanyama yakiwaning'inia, uchi wa mnyama jinsi walivyokuja duniani, na hawakujua hayo. Lakini walipompokea Kristo, na kuanguka kifudifudi na kumpokea Roho Mtakatifu, waliinuka na kukunja mikono yao wakificha aibu katika vifua vyao, huku wakiondoka na kutafuta nguo za kuvaa. Kwa nini? Wamekuwa wasafiri na wageni kwa ulimwengu huu. Haleluya! Wamekuwa mbali na hayo. Ndiyo, bwana.

43 Loo, ndiyo, watu hawa wajiita Wakristo. Ni washiriki wa makanisa. Wanaondoka na kusema, "Sisi ni Wamethodisti. Sisi ni Wabatisti. Sisi ni Wapentekoste. Sisi ni Wasabato. Sisi ni *hiki, kile,* na *kingine*." Haya hayahusiani hata sehemu moja na hili. Roho yako, ule uhai uliomo ndani yako, unakuhuisha na kukueleza wewe ni nani. Yesu alisema, "Kwa matunda yao mtawatambua."

44 Kanisa limekuwa kama Israeli hapo mwanzoni. Waliona mataifa yote ya makafiri wakiwa na mfalme. Mungu alikuwa mfalme wao. Na walipoona mataifa ya makafiri wana mfalme, ndipo walipenda kutenda kama hayo mataifa kafiri, nao wakajipatia mfalme. Na walipofanya hivyo, waliingia katika taabu. Polepole ulianza kuingia. Polepole ulimwengu ulianza kupenya ndani yao. Hatimaye uliishia kwa Ahabu. Mfalme mmoja akisogea karibu zaidi kidogo na huo, karibu zaidi kidogo na huo, hatimaye ulikamua ule uhai wote kutoka ndani yao. Na hapo wakapotoka. Na wakati Mfalme halisi alipokuja, hawakumtambua Yeye.

45 Hivyo ndivyo kanisa limefanya. Lilikubali. Mko hapa. Limekubali siasa, elimu. Limekubali madhehebu, mashirika, makanisa makubwa ya juu, wakiwatawisha wahubiri wakuu. Na wakati yule Mfalme halisi ajapo, Yeye hawamjui, nao wanamsulubisha Roho Mtakatifu hasa ambaye ni Mfalme wao. Hawamjui Yeye, lakini wanamcheka na kumfanyia

dhihaka. Kama Wayahudi walivyomfanyia Masihi wao, kanisa wanamfanyia Masihi wao namna hiyo hiyo. Hawajui hilo. Hawana macho ya kiroho, kwa sababu wamefundishwa mno kwa macho yao na wanachokiona, majumba makubwa, wakijaribu kujilinganisha na ulimwengu. Kamwe hatushauri—hatushauriwi kujilinganisha na ulimwengu. Tunashauriwa kujinyenyekeza wenyewe.

46 Na mmoja ndiye walio wengi kwa Mungu. Na leo katika wainjilisti wa uponyaji huko viwanjani, kuna mashindano makali, washindani. Mmoja asema, "Naam, Mungu asifiwe, ninao maelfu kadha. Ninao mkutano mkubwa kuliko ulio nao." Hilo linaleta tofauti gani? Tunaye mmoja au milioni moja, inaleta tofauti gani? Je sisi ni waaminifu kwa Mungu? Je! sisi ni waaminifu kwa Neno Lake? Je! tunastahimili chini ya jaribio la Roho Mtakatifu? Je hiyo ni kweli? Hilo ndilo jambo kuu.

47 Lakini tunapatana juu ya Biblia. Wengi wa watu wetu wa Kipentekoste, juu ya Mafundisho ya kimsingi ya Biblia hii, hupatana. Wapi. . . Sipendi kuwaumiza mawazo. Niko katika kanisa langu, na naona kwamba ninge—ningeweza kufanya tu vile katika kanisa langu, kwa sababu ninahubiri Injili. Lakini wapo makumi elfu ya wahubiri wa Kipentekoste wanaojua kwamba katika Biblia hakuna kitu kama ubatizo kwa jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Namhimiza askofu mkuu, au yeyote yule, anionyeshe mahali ambapo mtu yeyote aliwahi kubatizwa kwa jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Lakini hupatana kwa sababu madhehebu yamefanya hivyo. Hakuna mtu hata mmoja katika Agano Jipya, na kwa miaka mia tatu baadaye, kwa historia, isipokuwa aliyebatizwa katika Jina la Yesu Kristo. Ni nini? Madhehebu. Hayo ndiyo yaliyofanya hivyo. Wakipatana!

48 Na leo wamewaondoa wahudumu wa mitaani wote katika mitaa. Wameondoa matari kanisani. Wameondoa utukufu wote kanisani, na kuleta mahubiri ya seminari, mahubiri hafifu ya ushungi wa jogoo, wote wameadibishwa sana katika shirika, na wanawake wao wanavaa kaptula na nguo zinazobana mwili sana, na wanaume wakivuta sigara, na kucheza kamari na kuzungumza dhihaka chafu. Ni aibu machoni pa Mungu! Najua hilo ni chungu, lakini wakati umefika wa mtu fulani kusema kitu fulani. Wakipatana, kulegea, kutenda kama ulimwengu!

49 Sijali kama nitasimama peke yangu, pasipo mtu yeyote ila Mungu pekee, nitahubiri Kweli ya Biblia ya Mungu na kuitetea. Kama nitakufa, bado nitasimama kwa ajili ya ile Kweli. Hakika. Tunahitaji Kweli. Nitajipima siyo kulingana na kanisa, bali kulingana na Neno la Mungu nataka kujipima.

50 Lakini Delila, uliona, alijua kuwa Samsoni ana nguvu. Na hakujua nguvu hizo zinakaa wapi. Asingeweza kusema hizo nguvu zilikuwa nini, lakini kulikuwa na aina ya nguvu kuu

ambazo Samsoni alikuwa nazo, naye alitaka kuzipata. Na, kama Delila, alidumu akimbembeleza Samsoni kwa urembo wake. Loo, alivaa kizinifu hasa. Na alitembea mbele yake kwa kumvutia kama baadhi ya vijana wadogo wa siku hizi, na—na wengineo, na wakati unapotenda kitu fulani, kuvua nguo zake, akijaribu kumbembeleza Samsoni.

51 Ni jambo lile lile ulimwengu umefanya kwa kanisa. Sasa ziko wapi Nguvu zenu kuu?

52 "Naam, ikiwa tutaunda dhehebu, hiyo itazivunja zile Nguvu." Kanisa la Katoliki limefanya hivyo.

53 "Lakini Wafilisti wanakujia, Samsoni," Na Mluteri akatoka.

54 Ndipo waliunda madhehebu tena. "Kama mtanifunga na kamba nyingine, itaniweza." Kwa hivyo wakamfunga.

55 "Na Wafilisti wanakujia, Samsoni." Ilitokea nini? Wesley alitoka na kuzikata zile kamba.

56 "Sasa umenidanganya wakati wote. Hujui kuwa nakupenda, Samsoni? Vema, niambie ukweli wa moyo wako."

"Vema, nifunge kwa kamba nyingine."

57 "Vema, sasa tutafanya hivyo." Ni kitu gani? Hiyo ni kamba ya kimadhehebu.

58 "Uniache mimi niwe huru, hata sina madhehebu. Hapo, nakwambia, nitavunjika." Ndipo wakatoka Wapentekoste. Nguvu zako ziko wapi?

"Wafilisti wanakujia." Naye akazikata zile kamba tena.

59 Lakini sasa ilitokea nini? Iliwapata Wapentekoste, Madaktari wakubwa wa Elimu ya Uungu kuwa wachungaji wao, watu wakuu. Wanayo mafundisho mengi na taratibu sawa na Wamethodisti au Wabatisti, au yeyote ya wengine wote waliyo nayo. Nenda katika kanisa na huwezi kusikia "amina," wamepoa sana sawasawa na kundi la Waeskimo kutoka Nchi ya Kasikazini. Baridi! Hawajali! "Na sasa Wafilisti wanakujia, Samsoni."

60 Wafilisti wanakujia, Amerika. Uko wapi ule umoja wa roho? Uko wapi umoja wa Pentekoste? Wa Assemblies of God, United, na Church of God, *hili, lile* na *jingine,* kila moja lina itikadi tofauti, hili lina *hiyo*, na hili lina *ile*. Tumegawanyika hivi kwamba unaweza kwenda katika mji kufanya mkutano wa uamsho, kama kanisa moja wataudhamini, wengine wote hata hawatauhudhuria. Wakoministi wanakujia, Amerika.

61 Ziko wapi Nguvu zetu? Uko wapi utukufu wetu? Ni kitu gani? Kwa sababu tumefuata hekima ya kibinadamu badala ya Nguvu za Mungu! Kwa nini, wamewapata wahubiri wetu na mambo ni mazito na magumu mno, mpaka wametuunda kimadhehebu hadi tumekuwa na mioyo migumu na shingo ngumu sana, hata watu, kamwe husikii vifijo kanisani tena.

Kamwe husikii mtu yeyote akilia. Dawati la waliaji limewekwa katika orofa ya chini. Hakuna utukufu tena katika kanisa. Jambo pekee tunalofanya ni kukaa nyuma tu washupavu kama tuwezavyo kuwa. Hatuko huru. Tumefungwa. Ibilisi, kwa pepo wake mamboleo, amelifunga kanisa la Mungu aliye hai. Hiyo ni kweli. Hakuna Nguvu tena katika kanisa. Hakuna uhuru tena. Watu wamekuwa wagumu mno na baridi! Naam, Mungu anaweza kuja miongoni mwa Wapentekoste, na kujionyesha kuwa Yeye ni Mungu, na kuthibitisha ishara Zake za kufufuka Kwake, hata haiwashtushi wao. Utukufu! Naam, ni fedheha! Natembea nchini kote, Mungu akitenda kazi, akifanya ishara, na watu wanakaa kitako, na, "Naam, nadhani hiyo ni sawa. Loo, najua hayo yanaweza kutendwa." Haiwatikisi wao! Kwa nini? Wamefungwa na Delila, ulimwengu. Wamefungwa kwa pingu.

62 Sasa wamewaingiza hata humo, wamewafunga kwenye muungano. "Wafilisti wanakujia, Samsoni." Utafanya nini juu ya jambo hilo?

63 "Loo, tunayo madhehebu makubwa." Hakika. "Tunao washirika wengi zaidi ya tuliowahi kuwa nao." Lakini yuko wapi Roho? Yuko wapi Roho Mtakatifu?

64 Hilo ndilo Ibilisi amefanya. Alilimbembeleza kanisa. Aliendelea kulimbembeleza kanisa, "Njooni kwangu, nitawapa maskani kubwa sana hapa kama tu mtafanya *hili*. Kama mtamwondoa huyo mhubiri mshupavu wa dini mliye naye, na kumpata mtu, Daktari wa Elimu ya Uungu ambaye anazo fahamu, tutawajengea kanisa zuri kubwa lenye utaratibu na tutakuwa kama wengine wao." Hamna aibu! Afadhali muwe na mtu ambaye hajui tofauti kati ya kahawa na maharagwe lakini aliyejazwa Roho Mtakatifu, asiyepatana, kwa Nguvu za Mungu.

65 Lakini limekuwa, loo, ngumu mno, hata maskini mtakatifu fulani anaweza kutokea katika mkutano na kunena kwa lugha au kupiga kelele kidogo, au kufanya kitu fulani, na wale wengine wote watatupa macho na kuangalia. "Hiyo ilikuwa nini? Naam, nashangaa kwa nini? Huyo lazima awe shupavu wa dini aliyeingilia mahali fulani." Mnajua hiyo ni kweli! Maskini mtakatifu fulani akiingia, afurahi sana kiasi cha kuinua mikono yake, na kulia na kumsifu Bwana, mtu atakayepiga yowe "amina" katika mahubiri ya Injili, na wale wengine wote watageuka nyuma kuona amesema nini. Hao ni Wapentekoste. Kuna nini? Ninyi mnaiga Wamethodisti, na Wabatisti; wao waliiga Wakatoliki; Wakatoliki waliiga kuzimu. Na, wote kwa jumla, wote wanafuata kuzimu! Hakika.

66 Delila amewambembeleza akawaingiza kwenye makanisa makubwa, maridadi, wahubiri wasomi, kuchukua tabaka bora. "Naam, unajua, *fulani* hapa chini ni milionea, kama tungemfanya ahudhurie kusanyiko letu! Loo!" Kama hajazaliwa

mara ya pili, basi hastahili kuwa hapo. Sijali kama anazo dola milioni. Kama ana Kadilaki arobaini, chochote alicho nacho, anapaswa kuzaliwa mara ya pili, aje ashuke azaliwe upya na ahuishwe na Roho Mtakatifu, na atokee hapo katika uzao mpya, akikoroma (samahani), akilia na kupiga yowe, na kuendelea kama wengine wote wanavyofanya, na baada ya hapo aishi maisha yanayothibitisha kuwa amempata Huyo. Amina. Hilo ndilo mnalohitaji.

67 "Samsoni, Wafilisti wanakujia." Wakoministi wanakujia. Ulimwengu unakujia. Ibilisi anakujia.

68 Wanarudi na kumwona Roho wa Mungu akitenda miujiza na kutenda mambo ya kufufuka Kwake, yale Yesu aliyoahidi, wanasema, "Unajua, nadhani Ndugu Branham ana ujuzi mkubwa wa kusoma mawazo. Mchungaji wangu alisema hayo ni ya Ibilisi."

69 Ninyi maskini, wanafiki, makafiri mliopotoshwa, nyote mlioadibishwa sana, enyi mbwa mwitu katika mavazi ya kondoo! Yesu alisema, "Kama mngalinijua Mimi, mngalijua na siku Yangu." Lakini mnalo kundi la akina Sauli wanaojaribu kuwafanya mfanane na ulimwengu.

70 Tunahitaji kundi la watu wa Mungu wasiopatana juu ya Neno, lakini wanahubiri ile Kweli na kusimama katika ubatizo wa Roho Mtakatifu.

71 Lakini ulimwengu umefanya nini? Umenyoa Nguvu zenu zote. Mlizaliwa Wanadhiri, Pentekoste, lakini ulimwengu hakika umenyoa Nguvu zenu. Sasa mmekuwa wagumu kama wale wengine wote.

72 Tutafanya nini? Itakuwaje? Kuna jambo moja la utukufu ambalo naweza kuwaza kumalizia somo hili.

73 Wakati Samsoni alipokuwa amefungwa! Hatuwezi kuwa na uamsho. Msikilizeni ndugu yetu mwaminifu, Billy Granham, "Uamsho katika siku yetu!" Msikilizeni Oral Roberts akipaza sauti, "Uamsho katika siku yetu!" Wasikilizeni wale wengine wote, "Uamsho katika siku yetu!" Twawezaje kuwa na uamsho wakati tumefungwa? Tumemfunga Roho Mtakatifu, kwa madhehebu yetu na mapokeo yetu, na hatuwezi kuwa na uamsho wa Roho Mtakatifu! Amina. Najua hiyo inachoma sana, kwa hali ya hewa, lakini hiyo ndiyo Kweli! Twawezaje kuwa na uamsho wa Roho Mtakatifu wakati mmefungwa hivyo na mna mioyo migumu! "Mfano utauwa," Biblia ilisema wangekuwa nao. "Mfano wa utauwa, lakini wangekana Nguvu Zake." Nguvu za nini? Nguvu za madhehebu? Nguvu za ulimwengu? Nguvu za kanisa? Nguvu za Roho Mtakatifu! Hapo ndipo mahali pa siri katika kanisa. Na wakati kanisa linachukua wahubiri wasomi, na majumba makubwa na umaridadi, badala ya Roho Mtakatifu wa mtindo wa kale, ni afadhali warejee kwenye utume tena. Amina. Kweli. Mtawezaje kuwa na uamsho wa Roho Mtakatifu,

na watu wanamzimisha na wanamfunga na wanamwogopa? Hapo ndipo shida ilipo.

74 "Wafilisti wanakujia." Lakini tumaini moja la baraka tulilo nalo, wakati Samsoni alikuwa gerezani . . .

75 Walifanya jambo gani kwanza walipomkamata? Walimfunga, kwanza. Walimwondolea nguvu zake, waliigundua siri yake. Waliigundua siri yenu. Ulimwengu uligundua siri yenu. Sasa ninyi wanawake nyote mnakata nywele zenu, mnaenenda kama ulimwengu. Ninyi wanaume nyote mnakwenda na kutenda kama ulimwengu. Yote ni sawa, kufanya mizaha na utani mchafu, na mnakwenda nje na kuvuta sigara chache, na kutembea na wake za majirani, na mengineyo yote kama hayo, vinywaji vidogo vya ushirikiano usije ukapoteza kazi yako. Afadhali nilale na njaa na nile mkate mgumu na ninywe maji, na nibaki msafi na mweupe mbele za Mungu, kuliko kupatana kwa ajili ya kazi yoyote. Hilo ni kweli. Kweli. Dumu wa kweli kwa Mungu.

76 "Samsoni, Wafilisti wanakujia." Maskani ya Branham, mwenendo wa ulimwengu unanyemelea miongoni mwenu. Vipi basi? Mmefunua siri yenu? Mmefunua hiyo siri ambayo Mungu aliwapa mlipokuwa mnagaagaa pale katika unga wa mbao miaka michache iliyopita? Mmeacha iwaponyoke kwa njia ya ibada za kirafiki na utaratibu? Jambo gani limewapata? Mungu anaweza kushuka na kutenda muujiza na kupitia moja kwa moja kwa wasikizi na kuwaambia watu siri za mioyo yao, na kila kitu, na kuponya wagonjwa na walioteseka, na kutenda ishara na maajabu, na kuhubiri Neno Lake kwa nguvu wawezavyo, kwa Roho Mtakatifu; na watu wanasema, "Naam, nadhani kuwa hiyo ni sawa. Tunafurahia kuisikiliza mara kwa mara, kama hatukuchoka mno." Hiyo ni Maskani ya Branham. Wafilisti wanakujia.

77 Wakati, ilikuwa ya kwamba Neno lilipohubiriwa, na watakatifu wa zamani wakiwa na machozi machoni mwao, wangesimama kwa miguu yao na kutembea, wakilia, labda hawasemi neno, wakizunguka tu mara mbili au tatu, na walikaa chini, wakiwa wamejazwa na Roho Mtakatifu! Neno liliwalisha wao! "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno litokalo kinywani mwa Mungu." Wafilisti wanakujia, Maskani ya Branham.

Wafilisti wanakujia, Mpentekoste.

78 Bila shaka, Wafilisti waliwapata nyinyi, wengine wote, muda mrefu uliopita wakati mlipojikaza mno kwa kuunda madhehebu, isiwezekane kuingia kitu chochote isipokuwa wewe ulikuwa Mpresibiteri, Mbatisti, Mmethodisti, Mkatoliki, au kitu kingine. Msingekuwa na cho chote cha kushirikiana na hao wengine wote.

79 Hivyo, uamsho katika siku yetu? Twawezaje kuwa nao wakati mpaji uamsho wa sikuzote amefungwa na ulimwengu? Mungu hataingia mahali ulipo ulimwengu, mnaweza kutegemea hilo tu. Mkishirikiana na ulimwengu, ndipo ni—ni wote kwa jumla. Wakati mnaacha ulimwengu uwanyemelee, mnakwenda kutenda kama ulimwengu, hapo mmekwisha. Lakini wakati mtakata kila pingu mtoke kwa ulimwengu na kumjia Mungu, Mungu atawatumia hadi mtakapokwenda kubemba tena.

80 Hilo ndilo tumaini pekee nililo nalo asubuhi hii, kwa kufunga Ujumbe wangu, ni hili, "Wakati Samsoni alipokuwa amefungwa, tita jipya la nywele liliota."

81 Mungu, tuma kwetu Kanisa jingine kabla tu ya wakati wa mwisho, ili kwamba Uweza wa Roho Mtakatifu uweze kuja ndani yake, katika madhihirisho ya Roho, na Marko 16 iweze kufuatana na Kanisa, Matendo 2:4, Matendo 2:38, yote hayo yatakuwa yakifuatana na Kanisa. Ishara na maajabu viambatane na mitume. Ishara kuu za kufufuka Kwake zifuatane nao. Wakati tuko gerezani, hakika Mungu anakuza nywele mahali fulani, kwa mauaji makuu ya mwisho. Na iwe wewe, rafiki yangu Mkristo uliyeko hapa asubuhi hii, na iwe kwamba, nguvu zako zimeanza kukua. Ninaomba kwamba Ujumbe huu asubuhi ya leo, na huko nje katika nchi ambazo huu utakwenda, nasadiki kwamba huu Ujumbe utasaidia kuleta zile vitamini katika miili yenu zitakazokuza Nguvu za kiroho tena katika maisha yenu tena.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu na tuombe.

82 Ee Bwana Mungu, Muumba wa Mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, na Mpaji wa kila kipawa chema na cha kiroho, chukua maneno haya asubuhi hii na uyaweke moyoni, na uyatie maji, Bwana. Jalia watu waombee mambo haya, kwa vile tunaona kwamba ulimwengu umelibembeleza kanisa, na hatimaye umegundua Nguvu zake, umegundua mahali pake pa siri, umegundua mahali inapokaa siri yake, na umeinyoa. Umewachukua watu waliokuwa hapo kale wakipiga kelele za ushindi, hapo kale walikuwa na ushindi, na umewanyoa, wakae nyumbani Jumatano usiku kutazama vipindi vya televisheni. Umeondoa ile shangwe mioyoni mwao, na kuwapa wao kuupenda ulimwengu kuliko wanavyompenda Mungu. Umewapa wao ulimwengu zaidi, kwa ajili ya mambo ya ulimwengu, tamaa zaidi ya anasa za ulimwengu kuliko kuwa na kuhubiriwa kwa Injili. Kama hakuna bendi kubwa na kufanya yasiofaa na kelele za shangwe na kufanya yasiyofaa, ndipo hawataki ile Injili ya kale, tena, ambayo huleta machozi ya shangwe kwa nafsi, ambayo huleta uponyaji wa Kiungu tena, ambayo hurejesha karama za kimitume kwa kanisa, ambayo humleta Kristo aliyefufuka, Masihi wa leo.

83 Lakini kama Israeli walivyokuwa wamefungwa na—na mfalme wao, hata wasiweze kumfuata Mfalme halisi; na Mfalme halisi, wakati Yeye alipokuja, hawakumtambua Yeye. Ndivyo ilivyo leo, Ee Bwana, Mfalme wa Utukufu ametokea kwa namna ya Roho Mtakatifu, na, Bwana, wao hawamjui. Wao hawatambui hilo. Wamejifunga mno kimadhehebu, hata kwamba hawajui hilo, kwa sababu halimo katika madhehebu yao. Bwana, hii ni kazi ya Ibilisi ambaye amefanya hivi kwa watu.

84 Jalia Samsoni wa Mungu, jalia walio wasafi moyoni, wale wanaotamani na kulia, na kusihi na kushikilia, jalia wadumu nayo, Bwana, mpaka hizi nywele mpya ziote, mpaka ije tena shangwe katika Sayuni, na litokee kundi ambalo laweza kutambua na kuelewa, ambalo laweza kumwona Masihi na Nguvu zilizofichwa ambazo ulimwengu umefichwa, ambazo hawataelewa sasa. Tujalie, Bwana, kwamba wataona hili. Maana twaomba haya katika Jina la Yesu, Amina.

> [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.] . . . nguvu sasa hivi,
> Ee Bwana, tuma nguvu sasa hivi
> Na umbatize kila mtu.
>
> Walikuwa orofani,
> Wote walikuwa na moyo mmoja,
> Wakati Roho Mtakatifu aliposhuka
> Aliyeahidiwa na Bwana wetu.
>
> Ee Bwana, tuma Nguvu Zako sasa hivi,
> Ee Bwana, tuma Nguvu Zako sasa hivi,
> Ee Bwana, tuma Nguvu sasa hivi
> Na umbatize kila mmoja.

85 Jinsi ninavyompenda! Atume tu Nguvu Zake! Walikuwa orofani, wote kwa moyo mmoja. Ulimwengu wote ulikuwa umetoka ndani yao. Walikuwa wamefanywa watupu, na Roho Mtakatifu akaja.

86 Leo wanasema, "Njoo, jiunge na kanisa, andika jina lako katika kitabu. Au inama chini useme, 'Namkiri Kristo kuwa Mwana wa Mungu,' inuka." Ibilisi hufanya jambo lile lile. Hakika. Ibilisi alibatizwa wakati Yuda alipobatizwa. Ibilisi alikwenda na kuhubiri Injili wakati Yuda alipokwenda na kuhubiri Injili. Lakini Ibilisi hakupata Roho Mtakatifu. Ndivyo ilivyo. Hapo ndipo Nguvu iliyofichwa ilipo, huo ufufuo, ambao unajua hakika, pasipo shaka yoyote. Amina.

87 Yuko hapa. Roho Mtakatifu yule yule, Huyo ambaye alikuwa juu ya Masihi, bado yuko juu ya Kanisa Lake. Haliachi kamwe. "Nitakuwa pamoja nanyi sikuzote, hata ndani yenu, mpaka ukamilifu wa dahari. Nitakuwa hapo. Kazi nizifanyazo Mimi, nyinyi nanyi mtazifanya. Zaidi ya hizo mtafanya kwa kuwa naenda kwa Baba Yangu."

88 Lakini ulimwengu unapatana katika hilo, "Loo, hizo ni siku zilizopita!" Jambo lile tu Ibilisi anataka mfanye. Wanawataka mpate viinimacho. Mungu anataka ninyi rnbatizwe. Mungu anataka ninyi. . . Unasema, "Loo, siamini yasiyofaa hayo yote hapo." Endelea na kuishi, endelea kuishi katika dhambi zako, ishi katika dhambi zako. Lakini hadi utakapooza, mpaka uoze kwa fikira zako, mpaka uoze kwa mtindo wako, na uhuishwe upya tena na uzaliwe mara ya pili, na huo Uhai mpya utakuwa tofauti kabisa na ule uliokwenda chini.

89 Mbegu ya mhindi huenda chini ikiwa manjano, ikachipuka ikiwa kijani kibichi. Huingia chini ikiwa ngumu, imefunikwa, ikachipuka ya kupindikana na ikipeperushwa na upepo. Loo, utukufu! Haleluya! Wakati upepo unaanza kupuliza, ile mbegu haiwezi kufanya chochote ila kujisogeza, kuhama, lakini lile—lile jani dogo hupepea na kufurahi, hivyo hukua, hujiimarisha lenyewe. Haliwezi kuwa jani mpaka hindi limekufa na kuoza. Siyo kufa tu; bali na kuoza. Haliwezi kurudi tena, bali uhai hutoka ndani yake.

90 Kama nilivyosema muda kitambo uliopita, kuzaa ni jambo la kuchukiza, kinyaa, uchafu, kinyaa cha vinyaa, lakini hapo ndipo uhai ulipo. Wakati unajihesabu kuwa wewe binafsi u kinyaa, unapohesabu kanuni zenu za imani za Methodisti, Batisti na Pentekoste ni kinyaa, na unakufa madhabahuni, ndipo Uhai mpya unaingia ndani. Roho Mtakatifu anakuinua ndani juu ya hayo, unamwona Mungu.

91 Tutamwona Yeye siku moja yenye utukufu. Siku moja ng'ambo ya fahamu za kibinadamu, tutamwona Yeye. Unaamini hilo? Pana siku ng'ambo ya fahamu za kibinadamu, huko yaningojea kesho yenye furaha.

92 Nilikuwa nimesimama hapa pembeni usiku uliopita, na nilifikiri nimemwona Rabbi Lawson. Wakati alipokuwa mahali hapa, na angenifikia kwa bakora yake kuukuu na kunivuta kwa shingo yake, kunishika shingo kwa bakora yake, akanivuta mimbarani, na kuimba ule wimbo, "Yaningojea mimi. . ." [Nafasi tupu kwenye ukanda—Mh.]

93 Jambo fulani lilitendeka! Lilitoa ulimwengu nje. Nilianza kuona mambo tofauti. Nimekuwa nikihofu mno jinsi hawa Waamerika wanavyotenda, kila mara, mwaka kwa mwaka nikiona wanawake na wanaume jinsi wanavyojiaibisha na kuingia katika dhambi, hata karibu nizimie, mara mbili au tatu, nikifadhaikia jambo hilo. Jana, nilimwambia Mungu, "Sitakuwa na fadhaa tena. Neno Lako lilisema mambo yangekuwa hivyo, lakini nitasimama katika ufa na kukemea hayo, kwa yote yaliyomo ndani yangu."

94 Hivi majuzi, nilisimama pale katika Green's Mill, pango langu, huko nyuma nyikani, nilikuwa nikiomba siku nzima. Na yapata saa tisa, jua lilikuwa likitua, nami nilikuwa nikisimama

kule juu nikitazama kule ng'ambo, nikatoka nje ya lile pango, juu ya jabali kubwa. Na nilikuwa nimesimama hapo, nikitazama upande wa Mashariki, nikimsifu Bwana. Na niliweza kuona jua likiteremka chini nyuma ya miti kule juu ya huo mlima, nilitazama ng'ambo ya lile genge hadi katika hayo mengine, na yana majani mengi, kulikuwa kutulivu kama iwezavyo kuwa. Nami nikasema, "Bwana, siku moja ulimficha Musa katika ufa wa mwamba, na ukapita kando yake, kwa sababu alikuwa amechoka. Lakini ulipita karibu naye, alisema 'ilionekana kama mgongo wa mwanamume." Nilisema, "Nifiche mimi katika ufa, Bwana." Yapata wakati ule, upande wangu mmoja, ukaja Upepo mdogo ukishuka katika vichaka. Uliendelea kuvuma, ukashuka karibu nami, Upepo mdogo ukishuka chini, ukashuka ukapitia katika miti. Nilisimama pale.

> Siku moja, Mungu pekee ajua ni wapi au ni lini,
> Magurudumu ya uhai wa kibinadamu yatasimama,
> Ndipo nitakwenda kukaa katika mlima Sayuni.
>
> Siku moja isiyoweza kufikiwa na fahamu za mwanadamu,
> Siku moja, Mungu pekee ajua ni wapi au ni lini, (Kutatukia nini? Atakwenda kufunga, magurudumu haya yote yakizunguka.)
> Magurudumu ya uhai wa kibinadamu yote yatasimama
> Ndipo tutakwenda kuishi katika mlima Sayuni
>
> Bembea chini, ewe gari zuri,
> Limekuja kunipeleka mimi nyumbani;
> Bembea chini, ewe gari zuri,
> Limekuja kunipeleka nyumbani.
>
> Ukifika kule mbele yangu,
> Limekuja kunipeleka mimi nyumbani;
> Mwambie Ndugu Bosworth, na marafiki wangu wote, pia,
> Limekuja kunichukua tu kunipeleka nyumbani.
>
> Sasa bembea chini . . . (litashuka chini siku fulani na kunichukua juu) . . . gar- . . .
> (Kila mti utawaka moto; Malaika wa Mungu na magari ya moto) . . . kunipeleka nyumbani;
> Bembea chini, ewe gari zuri,
> Limekuja kunipeleka mimi nyumbani.

95 Mojawapo ya siku hizi, mojawapo ya siku hizi katika sehemu ya chini zaidi ya saa za kufa kwangu, namtazamia Yeye aje. Hiyo ni kweli.

Nilitazama ng'ambo ya Yordani nikaona nini
Limekuja kunipeleka nyumbani; (kama mzee
  Eliya akitazama ng'ambo ya Yordani)
Kundi la Malaika wanaong'aa wanakuja
  kunichukua,
Walikuwa wanakuja kunipeleka nyumbani.

Bembea chini, shuka chini, ewe gari zuri,
Limekuja kunipeleka nyumbani;
Bembea chini, ewe gari zuri,
Limekuja kunipeleka nyumbani.

96 Bwana Yesu, Dreva mbarikiwa wa gari hili, Nahodha wa meli ya kale ya Sayuni, mashua ya Uzima, anazunguka katika hili jengo, akinena, Uwepo Wake uko hapa. Roho Mtakatifu hasa aliyemwinua Yeye kutoka kaburini yuko hapa.

97 Kwa vile hawakutoa kadi za maombi, je kuna mtu yeyote asiyetoka humu mjini, ambaye simfahamu, ambaye yuko hapa ili aombewe? Inueni mikono yenu, wale ambao siwafahamu. Inueni mikono yenu juu, nisiowafahamu. Wewe, wewe hapo. Naamini huyo jamaa mdogo mwenye masharubu hapo nyuma, mtu fulani aliinua mkono wake nyuma upande ule. Ndiyo, wewe, je uliinua mkono wako? Sawa. Nyuma kule, wewe, bwana. Sawa. Ninyi nyote ni wageni Kwangu? Huyo Bwana Yesu, yeye yule Mchungaji wa kundi la kondoo hapa, je mnaamini ahadi Zake ni kweli? Analipaka mafuta kanisa Lake na "Kazi nizifanyazo mimi, ninyi nanyi, mtafanya. Hata kubwa kuliko hizo mtafanya, kwa kuwa naenda kwa Baba. Zaidi ya hizi!" Mnaamini hilo?

98 Je uliinua mkono wako kwamba hukunijua mimi? Je unaamini Mungu anaweza kuniambia yaliyoko moyoni mwako, anaweza kuzungumza na mimi kama vile tu alivyofanya kwa yule mwanamke aliyegusa vazi Lake? Je unaamini Yeye ni Kuhani Mkuu ambaye anaweza kuguswa na mambo yetu ya udhaifu? Kama Mungu atanifunulia mimi hali zako, utaamini kuwa mimi ni nabii Wake, utaamini kwamba Uwepo Wake uko hapa na ndiyo maana anaruhusu haya? Unaomba kwa ajili ya mke wako. Ana nyonga iliyovunjika, nyonga iliyotenguka. Hiyo ni kweli. Kama ni kweli, simama. Vema, nenda ukamkute, mwenye afya. Amina.

99 Vipi kuhusu wewe hapo nyuma, jamaa mdogo ambaye alisimama, ambaye alikuwa na masharubu? Je unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako? Unaamini mwanao atakuwa mzima? Unaamini? Unaye mvulana, ambaye akili zimeoza. Hiyo ni kweli. Wewe siyo... Unatoka Kentucky. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako juu. Mimi sikujui, sivyo? Kama mimi si... Inua mikono yako namna *hii*, hatujuani mimi na wewe. Hiyo ni kweli. Ni kumtegemea Mungu. Je unaamini? Kama unaamini, utampata mvulana wako jinsi unavyoamini. Weka tu hilo katika moyo wako.

100 Ni nani hapa waliinua mikono yao, ya kwamba siku—siku . . . Ni wewe? Vema, bwana, unaamini kuwa mimi ni nabii wa Mungu? [Yule mtu anasema, "Amina"—Mh.] Unaamini, kwa moyo wako wote? Hakuna haja kuinuka, simama tu papo hapo. Vema, bwana, shida yako, una kisukari. ["Hiyo ni kweli"] Na kinasumbua mguu wako. ["Ndiyo"] Unatoka Ohio. ["Ndiyo"] Jina lako ni Bw. Miller. ["Hiyo ni kweli"] Rudi nyumbani na uwe mzima. Vema, amini kwa moyo wako wote. Vema.

Unaamini hilo? Kama unaweza kuamini!

101 Bibi ambaye amekaa hapa, je uliinua mkono wako? Bibi mnene, aliyevaa miwani, unaamini kwa moyo wako wote? Unaamini hili? Unaamini mimi ni mtumishi wa Mungu? Unaamini? Vema, kama Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini, je utaamini? Shida ya moyo. Vema, inua mkono wako kama hiyo ni kweli. Vema.

102 Bibi hapa wa pili kwako, aliinuka. Moyo; lakini hasa ni macho yako. Namjua huyu. Vema, kama unaweza kuamini!

103 Nyuma pale, mwanaume wa pili pale nyuma ana tatizo la moyo, pia, na ugonjwa wa ngozi. Je unaamini kwamba Mungu atakufanya mzima? Unaamini, bwana?

104 Kuna mwanaume nyuma pale mahali fulani, aliinua mikono yake kwamba sikumju . . . Bw. Schubert. Vema, bwana. Vema, unaamini? Ni kwa ajili ya macho yako, pia, sivyo? Unaomba kwa ajili ya mama yako ambaye amekaa kule nje, pia. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Sisi hatujuani. Hiyo ni kweli? Peana mikono, peaneni mikono nyinyi kwa nyinyi. Vema, hiyo ni sawa. Kama mnaweza kuamini, mnaweza kupokea!

105 Yesu Kristo aliyefufuka yuko ndani ya hili jengo. Ni Mtu yule yule. Inawafanyia nini? Mmeacha ulimwengu unyonye nguvu zote kutoka ndani yenu? Utukufu! Napenda uzao mpya! Napenda Uhai mpya! Sijali unakuja kwa ndege ipi, iwapo itanibidi kuwa mtakatifu avingirikaye, lolote. Sijali anakuja kwa ndege ipi, nahitaji Roho Mtakatifu halisi kama aliye juu yangu sasa. Nataka kumhifadhi Huyo! Ni heri niwe Naye kuliko vitu vyote vya ulimwengu huu. Amina! Mnaamini? Je mnaamini Yeye yuko hapa?

106 Wekeni mikono yenu kila mmoja juu ya mwenzie, basi. Niambie ni jambo gani zaidi angeweza kutenda. Hakuna. Muwe na imani sasa. Aminini yamekwisha.

107 Bwana Mungu, Muumbaji wa Mbingu na nchi, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, na Mpaji wa vipawa vyema vyote, Roho Wako yuko hapa katika upako, Bwana, inaonekana kama hili jengo linapumua, linayumbayumba. Kwa nini watu wasiweze kuelewa hili, Bwana? Wao wa—wamejishirikisha na ulimwengu mno, mpaka wamepoa na kushika desturi na wenye mioyo migumu sana, hata hawawezi kukujua Wewe tena? Bwana Mungu, jalia Nguvu hii imguse kila mmoja, na kila mgonjwa

aponywe, kila mwenye dhambi aokolewe, na Mungu apate utukufu. Katika Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, naomba haya. Amina.

108 Mnaamini haya? Inueni mikono yenu. Mnakubali uponyaji wenu? Mungu awabariki. Sasa nendeni na mtayapata jinsi mnavyoamini, itakuwa hivyo. Naona maono yakiwatokea wengine. Hiyo ni kweli. Yanibidi kurudi usiku wa leo.

109 Kama huamini sasa, hutaamini kamwe. Hiyo ni kweli. Yesu alifanya hivyo safari moja, na walisema, "Wewe ni . . . Sisi tunajua wakati Masihi atakapokuja, Yeye atatwambia haya." Akasema, "Najua Masihi atafanya hayo. Lakini Wewe ni Nani?"

Yeye alisema, "Mimi Ndiye."

110 Ndipo akakimbilia mjini na kusema, "Njooni, mmwone Mtu aliyejua nilivyokuwa na mambo niliyofanya. Je huyu siye Masihi?"

111 Yeye alisema, "Mambo haya yatatokea tena katika siku za mwisho. Kanisa litakuwa likihubiri ile Kweli, litakuwa likisimama katika Neno. Litakuwa linatenda Amri zote za Mungu. Halitashirikiana na ulimwengu. Na kupitia hapo nitaenenda na kufanya mambo yale yale."

112 Lakini Yeye alisema, "Watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wenye mfano wa utauwa," watu wa dini sana, waendao makanisani. "Wenye mfano wa utauwa, lakini wakikana Nguvu zake. Hao nao ujiepushe nao!"

113 Ninyi watu, kokote mlikokuwa ndani ya kanisa, aliowaita Yeye sasa hivi, maono yameondoka kwangu. Kama—kama hayo yalikuwa kweli, niliyosema, na mimi ikiwa sijui mambo yenu hayo, inueni mikono yenu, mtu awaye yote. Kote kanisani, kila—kila mahali. Vema. Unaona? Siwajui hao, sijawahi kuwaona; lakini Roho Mtakatifu yuko hapa na Yeye anawajua. Je hamwezi kuona kwamba siyo mimi?

114 Sikiliza! Ikiwa Yeye ataniaminisha hayo, Yeye ataniaminisha kwa Kweli ya Neno, kwa sababu ile Kweli inaweza kuja tu kwa Neno. "Tubuni, kila mmoja, mkabatizwe kwa Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Mnaamini hilo? Kutakuweko na ibada ya ubatizo baada ya muda mfupi.

115 Hebu tuinamishe vichwa vyetu. Nitamwomba mchungaji asali wakati wanajiandaa kwa ajili ya ubatizo. Nafikiri kuna ibada ya ubatizo inayofuata. Vema.

*Kanisa Halisi*
(*The Church*)

Jumbe hizi za Ndugu William Branham, zilihubiriwa hapo awali katika Kiingereza kwenye Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2009.

SWAHILI

©1991 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org